# MKATABA WA NUNUA LEO LIPA BAADAYE (NLLB/BNPL)

**Wahusika wa Mkataba**
**Sokowatch Company Limited** wa S.L.P 106092 Mikocheni Dar Es salaam, Ni Kampuni iliyosajiliwa kwa sheria za Makampuni Tanzania na yenye leseni ya kufanya biashara Tanzania (Hapa itafahamika kama Wasoko). Mteja na Wasoko kwa pamoja watafahamika kama "Wahusika wa Mkataba"

**Kuzingatia**
Kwa kuzingatia kampuni ya Wasoko kuwasilisha bidhaa zilizoagizwa kwa mkopo (NLLB) kwa mteja, mteja anakubali kulipa kiasi kilichoainishwa cha bidhaa pamoja na ada nyingine zote zikiwemo ada ya kupewa mkopo na ada za ucheweleshaji kama mteja atachelewsha malipo kama ilivyo ainishwa na kampuni ya wasoko kabla ya au tarehe husika ya kulipa.

**Kiasi cha bidhaa za NLLB zilizowasilishwa na malipo.**
Kabla ya agizo la bidhaa kuwekwa, Wasoko itamjulisha mteja kiasi kikuu kitakacholipwa kwa bidhaa zilizoagizwa kwa mkopo. Wasoko pia itamjulisha mteja wakati ada zozote zikiwemo za kupewa mkopo na za ucheweleshwaji zikifikia na zinatakiwa kulipwa. Kwa maswali yoyote kuhusu kiasi kinachotakiwa kulipwa mteja anapaswa kushauruiana na wafanyakazi wa Wasoko anaowasiliana nao kabla ya kuagiza bidhaa. Order ya mkopo na bidhaa zilizoagizwa kufikishwa kwa mteja, mteja atakagua bidhaa zilizopelekwa na kama zitakuwa sawa basi atakubali kwa kumpatia nywila (OTP) ambayo ataipata kwa njia ya sms, kwa kukubali huko kunajumuisha kukubalika kwa kiasi chote cha mkopo kinachodaiwa ikiwa ni pamoja na ada kupewa mkopo na ada ya ucheweleshaji ya siku zijazo kama mteja atachelwesha malipo yake ya mkopo.

**Malipo,**
Malipo yote ni lazima yawasilishwe kwa njia ya lipa number ya Vodacom, ambayo ni 816222. Wasoko hawatawajibika kwa hasara yoyote itakayotokana na malipo ya fedha taslimu yaliyofanywa na mteja kwa mfanyakazi, kwani wafanyakazi wote wa Wasoko wamepigwa marufuku kabisa kupokea na kufanya miamala ya pesa taslim kwa ajili ya mauzo ya mikopo amabyo inatakiwa ifanyike kupitia utaratibu uliowekwa.

**Tukio la kutokulipa deni**
Kama mteja akishindwa kulipa deni kufikia tarehe zilizotajwa, Wasoko inaweza kutumia ada ya ucheweleshaji au malipo ya kiasi cha msingi ili kufanikisha deni kulipwa, Wasoko wanaweza kuingia makubaliano na makampuni yanayohusika na ukusanyaji wa madeni ili yasidie kwenye kukusanya madeni yake endapo mteja atakuwa msumbufu na Wasoko kushindwa kummudu. Ada zilizopatikana katika mchakato wa kurejesha deni hili zikiwa ni pamoja na ada za kisheria na za kampuni ya ukusanyaji wa madeni zitaongezewa kwenye deni lako, ili izilipe pamoja na deni hilo.

**Masharti ya kupata huduma ya mkopo.**
Wasoko inahifadhi haki wakati wowote, bila idhini au notisi kwa mteja, kughairi au kurekebisha ufikiaji wa mteja kwa mkopo na mipaka yake.

**Kurejesha umiliki**
Wasoko inahifadhi haki ya kuingia katika eneo au makazi ya Mteja na kuchukua umiliki wa bidhaa iliyopelekwa kwa Mteja kama njia ya kukusanya malipo yoyote ambayo Wasoko inamdai Mteja. Wasoko inahifadhi haki ya kuuza bidhaa husika baada ya kuzichukua ili kukamilisha malipo yoyote ambayo Mteja anadaiwa na Wasoko.

**Kusitishwa kwa makubaliano**
Wasoko anaweza kusitisha Makubaliano haya bila kutoa notisi kwa Mteja. Baada ya kusitishwa kwa mkataba huu, Mteja atalipa deni lolote analodaiwa au kiwango cha deni kilichobaki kwa Wasoko. Mteja anaweza kusitisha Mkataba huu baada ya kumaliza malipo ya bidhaa zilizochukuliwa kwa mkopo kwa kuzingatia utaratibu wa Wasoko wa kuchukua umiliki wa bidhaa husika.

**Masharti ya kupata mkopo wa bidhaa**
Wasoko inahifadhi haki ya kusitisha au kurekebisha upatikanaji wa mkopo kwa Mteja na viwango vya mkopo, wakati wowote bila ridhaa au notisi kwa Mteja.

**Kusitisha huduma**
Wasoko inahifadhi haki ya kusitisha kutoa huduma bila kutoa notisi kwa Mteja, endapo kutakua na malipo yaliyocheleweshwa na Mteja.

**Dhamana (Warranties)**
Mteja anawakilisha (represents) na kuthibitisha (warrants) kwa Wasoko wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu kwamba:

- hajashawishiwa kuingia katika Mkataba na kwamba kuingia kwake katika Mkataba huu hakutegemei taarifa au maelezo yoyote au maoni au uwakilishi, uhakikisho, au dhamana isipokuwa kama ilivyoonyeshwa katika Mkataba huu, na Mteja bila masharti yoyote amekubali kuachilia haki yoyote ya kudai fidia kwa uwakilishi, taarifa au maelezo yoyote (nje ya au ndani ya Mkataba huu) dhidi ya ukiukaji wowote wa dhamana (warranty) yoyote ambayo haipo katika Mkataba huu, isipokuwa pale ambapo uwakilishi au dhamana kama hiyo ilifanywa au kutolewa kwa njia ya ulaghai, na au kubatilisha Makubaliano;

- Wajibu wake chini ya Makubaliano ni wajibu wa kisheria, halali, unaofunga(binding), unaoweza kutekelezwa dhidi yake kwa mujibu wa vipengele husika;

# MKATABA WA NUNUA LEO LIPA BAADAYE (NLLB/BNPL)

- ana uwezo na mamlaka ya kuingia na kutekeleza na kutimiza wajibu wake chini ya Mkataba huu;

- hatua zote, masharti na mambo yanayohitajika kuchukuliwa, kutimizwa na kufanywa na Mteja (ikiwa ni pamoja na kupata ridhaa na uidhinishaji unaohitajia) kwa ajili ya kuingia na kutekeleza Mkataba huu zimechukuliwa, zimetimizwa, na kufanyika;

- Kuingia kwake na kutekeleza Mkataba huu hakukiuki sheria yoyote ambayo Mteja yuko chini yake; na

- kwamba taarifa yoyote iliyowasilishwa kwa Wasoko ni sahihi na kamili na itakuwa, kwa kadiri ya ufahamu na imani yao, kamili na sahihi. Endapo kutakua na mabadiliko yoyote ya msingi (material) katika taarifa husika, Mteja atamjulisha Wasoko mara moja kwa maandishi kuhusu mabadiliko hayo.

- Kwamba amekagua na kujiridhisha kwamba bidhaa zinafaa kwa matumizi yanatorajiwa na kwamba Wasoko haitawajibika kwenye madai yoyote yanayohusika na ubora au kufaa kwa bidhaa husika

**Ukusanyaji wa taarifa (Data)**
Wasoko itaomba taarifa (data) binafsi za mteja kama sehemu ya kumjua mteja wake (KYC). Taarifa hizi zinaweza kujumuisha utambulisho wa kibinafsi wa kibiashara. Mteja anakubali Wasoko kutumia na kuchakata data za kibinafsi.Mteja atahakikisha kwamba maagizo yote na data za kibinafsi zilizotolewa kwa Wasoko ni za mteja na ni sahihi.Mteja ana wajibu wa kumjulisha Wasoko mara moja kusahihisha taarifa zake au taarifa yoyote iliyotolewa kimakosa chini ya makubaliano haya pindi mteja anapofahamu hitilafu kama hiyo.

**SMS na simu kwa mteja.**
Mteja anaweza kupokea simu na SMS kutoka kwa Wasoko zenye salio linalodaiwa, njia ya malipo, tarehe ya kufanya malipo na taarifa nyingine yoyote kutoka kwa Wasoko.

**Kiziuzi cha deni.**
Wasoko kwa kukosekana kwa uzembe mkubwa au utovu wa nidhamu wa makusudi, hawatawajibika kwa hasara yoyote au uharibifu utakaompata mteja au mtu mwingine yeyote, unaotokana na utekelezaji wa Wasoko wa haki zozote chini ya makubaliano haya au uvunjaji wowote wa mteja wa majukumu yake chini ya mkataba huu. Mteja atamjulisha Wasoko dhidi ya dai lolote la mteja au mtu mwingine yeyote litakalojitokeza.

**Utatuzi wa migogoro**
Wasoko na Mteja watasuluhisha madai, masuala, sintofahamu na migogoro itakayoibuka kuhusu mkataba huu kwa njia ya majadiliano. Endapo njia ya majadiliano itakwama kutoa ufumbuzi wa masuala tajwa, upande wowote utakua na haki ya kuwasilisha madai, sintofahamu au mgogoro huo katika mahakama yenye mamlaka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Sheria inayosimamia Mkataba**
Mkataba huu utasimamiwa, kufafanuliwa na kutasfiriwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Upekee wa vifungu vya Mkataba (Severability)**
Kila kifungu cha Mkataba huu kinasimama pekee kwa kujitegemea bila kuathiri vifungu vingine. Endapo kifungu chochote cha Mkataba huu kitaonekana kuwa batili au kisichotekelezeka basi ubatili au kutotekelezeka huko hakutaathiri vifungu vingine vya Mkataba huu.

**Utekelezaji na tarehe ya Makubaliano**
Mkataba huu utaanza katika tarehe iliyoonyeshwa hapa chini na utaendelea kutumika katika kila maombi ya mkopo kwa mteja kama yalivyoelezwa hapa chini.